

Taarifa ya Mwaka
2013
Annual Report

Contents





Yaliyomo

1. Financial Highlights Vielelezo Muhimu vya Kifedha	2	• Statement of Profit or Loss and other comprehensive income Taarifa ya Faida au Hasara	52
2. Value Added Statement Taarifa ya ongezeko la thamani	6	• Statement of Financial Position Mizania	53
3. Mission, Vision and Values Azma, Dira na Maadili	7	• Statement of Changes in Equity Taarifa ya mabadiliko ya Mtaji	55
4. History and Ownership Historia na Umiliki	8	• Statement of Cash Flows Mtiririko wa Fedha	56
5. Board of Directors Bodi ya Wakurugenzi	12	• Notes to the Consolidated Financial Statements Ufafanuzi wa Taarifa za Hesabu	58
6. Chairman's Report Taarifa ya Mwenyekiti	16	14. Risk Report Taarifa ya Athari	106
7. Chief Executive Officer's Report Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu	20	15. Executive Management Uongozi wa Juu	109
8. Corporate Governance Utawala Bora	32	16. Key Management Committees Kamati za Menejimenti	113
9. Sustainability and Corporate Social Responsibility Uendeleu na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii	38	17. Distribution Network Mtandao wa Huduma	115
10. Report of the Directors Taarifa ya Wakurugenzi	43	18. Annual General Meeting Notice 2014 Taarifa ya Mkutano Mkuu wa mwaka 2014	116
11. Statement of Directors' Responsibilities Taarifa la Wajibu wa Wakurugenzi	49	19. Company Information Taarifa za Kampuni	119
12. Independent Auditor's Report Taarifa ya Wakaguzi wa Hesabu	50	20. Key Contacts Anuani Muhimu	120
13. Financial Statements Taarifa za Hesabu	51	21. Whistle Blowing Kutoa Taarifa	121





1 Financial Highlights | Vielelezo Muhimu vya Kifedha

Highlights for the Financial periods 2009 - 2013
Mambo muhimu kwa vipindi vya fedha 2009 - 2013





BALANCE SHEET



INCOME STATEMENT



RATIOS



KEY FIGURES FOR THE PERIOD 2009 - 2013 Takwimu muhimu vipindi vya 2009 - 2013						
		2009	2010	2011	2012	2013
Profitability						
Total Income	Tzs Million	167,933	199,999	266,594	359,138	422,171
Tax	Tzs Million	20,488	24,464	30,947	47,340	54,225
Operating expenses	Tzs Million	92,870	119,880	152,056	198,934	225,298
net profit	Tzs Million	47,550	53,981	71,839	97,401	133,906
Solvency						
Total Assets	Tzs Million	1,669,333	2,110,903	2,170,250	2,795,878	3,280,186
Tier 1 capital	Tzs Million	187,804	220,215	270,470	329,688	421,804
Risk Weighted Assets (RWA)	Tzs Million	792,186	960,418	1,273,282	1,565,509	1,944,390
Other						
Customers		1,424,015	1,583,918	1,803,203	1,782,869	2,287,958
Branches		134	139	140	147	153
ATMs		281	345	416	473	485
Staff		2,478	2,610	2,650	2,702	2,783

Selected ratios	2009	2010	2011	2012	2013
Return on average shareholders' equity	27%	26%	28%	27%	29%
Return on average assets	3%	3%	3%	3%	4%
Cost to income ratio	55%	60%	57%	55%	53%
Capital adequacy ratio *	24%	23%	22%	21%	22%
Dividend per share	31	36	50	68	90

* Regulatory requirements for Tier I and II are 10% and 12% respectively

* Capital adequacy ratios are calculated before dividend payments

SHARE PERFORMANCE Mwenendo Wa Hisa	FORMULAS Fomula	UNITS	2009	2010	2011	2012	2013
Basic and diluted earnings per share	PAT/Number of shares in issue	Tzs	95	108	144	195	268
Dividends per share	Total dividend/ Number of shares in issue	Tzs	31	36	50	68	90
Closing share price	as per DSE	Tzs	810	660	850	1,120	2,620
Number of shares in issue		Millions	500	500	500	500	500
Dividend cover (times)	Basic diluted earnings per share/dividends per share		3.03	3.00	2.87	2.87	2.98
Net asset value per share	Net assets /Number of shares in issue	Tzs	384	461	569	714	913
Dividend yield - ordinary dividend	Dividend per share/ closing price at DSE	%	4	5	6	6	3
Earnings yield - ordinary dividend	PAT/closing share price	%	12	16	17	17	10
Price to Book ratio	Closing share price/ Net Asset Value per share		2.11	1.43	1.49	1.57	2.87
Price: Earnings ratio - ordinary shares	Basic diluted earnings per share/closing share price		8.52	6.11	5.92	5.74	9.78
Market capitalisation	Closing share price times No. shares in issue	Tzs Millions	405,000	330,000	425,000	560,000	1,310,000
Net Assets	Audited Financials	Tzs Millions	192,239	230,520	284,359	356,954	456,666
Volume of shares transacted	DSE	Millions	20.7	6.4	23.0	8.7	11.0
Exchange weighted share price (Tzs)	DSE	Tzs	805	758	786	954	1,891

Value added statement | Taarifa ya Ongezeko la thamani



Value added statement for the year ended 31 December 2013

Value added is the wealth the bank has been able to create by providing clients with a quality, value added service.

Taarifa ya ongezeko la thamani kwa mwaka ulioishia Disemba 2013

Ongezeko la thamani ni mali ambayo benki imeweza kujitengenezea kwa kumpatia mteja huduma yenye ubora na ongezeko la thamani.

TZS 'MILLIONS	2013		2012	
Value added				
Ongezeko la thamani				
Income earned by providing banking services Mapato yaliyoyotokana na huduma za kibenki	448,064		368,486	
Cost of service Gharama ya huduma	(49,659)		(35,199)	
value added by banking services Ongezeko la thamani kwa huduma za kibenki	398,405		333,287	
Non operating income and operating expenses Mapato yasiyo ya gharama za uendeshaji na matumizi	(110,599)		(111,107)	
	287,806		222,180	
Value allocated				
Thamani zilizotengwa kwa ajili ya:				
To employees:				
Wafanyakazi				
• Salaries and other benefits • Mishahara na marupurupu mengine	99,675 35%		75,955 34%	
To shareholders:				
Kwa wanahisa				
• Dividend to the shareholders • Gawio kwa wanahisa	34,000 12%		25,000 11%	
• of which to government • ambayo kwa Serikali ni	10,805		7,945	
To Government:				
Kwa Serikali				
• Income Tax • Kodi ya Mapato	54,225 19%		49,623 23%	
• PAYE • Kodi ya Ajira	20,632 7%		14,203 7%	
• SDL • Ushuru wa ujuzi wa maendeleo	4,706 2%		4,557 2%	
To other stakeholders (Sponsorship/Donations):				
Kwa wadau wengine (Udhamini/Misaada)	1,049 0%		891 0%	
To expansion and growth:				
Upanuzi na Ukuaji wa benki				
Depreciation, deferred tax and retained earnings Uchakavu, kodi zinazotofautiana na mapato yaliyobakizwa	73,519 25%		51,951 23%	
	287,806 100%		222,180 100%	



Mission, Vision and Values

Azma, Dira na Maadili

Our Mission

Through innovative distribution and our extensive branch network, to offer affordable customer focused financial services to the Tanzanian community, in order to realise sustainable benefits for all our stakeholders

Our Vision

To be the preferred financial services partner in Tanzania

NMB Values

WHAT DRIVES US

■ Eagerness

We have a strong desire to show our best as we believe that NMB is the right place to grow to our full potential. We are always looking for opportunities/innovations and we will not run away from problems as we recognize the challenge of overcoming them.

■ Ownership

We feel responsible for our own tasks so we plan our work; do our own quality control and we will not rest before we fulfill our goals. We also take ownership for a clean and safe environment, and the general well-being of NMB, no matter in which area we work.

WHAT BINDS US

■ Customer focus

We focus on the needs of our internal and external customers and stakeholders by offering our support, manage expectations, doing what needs to be done and check satisfaction afterwards. We realize that we should always act as ambassadors of our brand and never forget that our customers pay our salary.

■ Teamwork

Our job is not finished as long as we can still support our colleagues. We share and are eager to learn best practices as we are open for suggestions from colleagues. We give and accept specific feedback in a constructive manner. We also feel that we are part of the NMB family and we celebrate together our successes as The Winning Team.

WHAT GUIDES US

■ Integrity

Integrity is our highest value. Customers and management should always be able to check and ask for proof and should never be disappointed and never rely only on 'trust'. We keep customer information confidential and report irregularities to management through whistle-blowing.

■ Compliance

We have full knowledge and understanding and always comply to internal and external regulations. We act in line with our code of conduct. If we are not able to comply, we escalate or complain internally. We act as professionals by not sharing passwords and taking full responsibility for mandatory controls. We act, speak and work professionally to avoid any mistakes derived from habitual incidents.

Azma Yetu

Kutumia ubunifu katika utoaji huduma na mtandao mpana wa matawi yetu ili kutoa huduma za kibenki kwa gharama nafuu zenye kumlenga mteja wa jamii ya Tanzania ili kuwa na manufaa endelevu kwa wadau wetu wote.

Dira Yetu

Kuwa mbia wa huduma za kifedha anayependelewa zaidi nchini Tanzania

Maadili yetu

KINACHOTUSUKUMA

■ Ari

Tuna azma kubwa ya kuonyesha uwezo wetu kwani tunaamini NMB ni mahali sahihi kwa ukuaji katika nyanja zote. Kila wakati tunaangalia fursa/ubunifu uboreshaji mpya na kamwe hatutakwepa matatizo kwani tunatambua changamoto zinazotukabili na tunazitafutia ufumbuzi.

■ Umiliki

Tunatambua majukumu ya kazi zetu hivyo tunazipangilia, tunasimamia ubora na kamwe hatutachoka hadi kufikia malengo yetu. Pia tunawajibika kuhakikisha mazingira ya kazi ni safi na salama.

KINACHOTUUNGANISHA

■ Tunamlenga Mteja

Tunalenga kukidhi mahitaji ya wateja wetu wa ndani na wa nje kwa kuwapa ushirikiano ili kukidhi matarajio yao, kutekeleza kile kinachotakiwa na kuangalia mafanikio ya baadae. Tunatambua siku zote tunatakiwa kuwa mabalozi wa NMB na bila kusahau wateja wetu ndio wanaotulipa mishahara yetu.

■ Ushirikiano Wetu

Kazi yetu haijakamilika ikiwa bado tunaweza kusaidia wenzetu. Tunashirikiana na tuna ari ya kujifunza mbinu bora na sahihi kwani tuko tayari kupokea maoni kutoka kwa wadau. Tunatoa na kupokea maoni kwa njia iliyo sahihi. Pia tunajiona wote ni sehemu ya familia ya NMB na tunasheherekea mafanikio yetu pamoja.

MIONGOZO

■ Uadilifu

Uaminifu ndio mwongozo wetu mkuu. Wakati wote Wateja na Uongozi wanatakiwa kuangalia na kupata Uthibitisho na kamwe wasikatishwe tamaa. Tunatunza siri za wateja wetu na kutoa taarifa mara moja kwa uongozi pale ambapo mambo hayaendi sawa.

■ Utimilifu

Tuna uelewa na ujuzi wa kutosha na siku zote tunafuata taratibu za ndani na nje ya Benki katika kutimiza wajibu wetu. Ikiwa tuna tatizo na kufuata taratibu za ndani kwa sababu za msingi basi tunaenda mbele zaidi na kutafuta ufumbuzi. Tunatekeleza kazi zetu kitaalamu kwa kubeba majukumu yote ya lazima ya kisheria kuepuka makosa katika matukio ya kila siku.



National Microfinance Bank plc (NMB) is one of the largest commercial banks in Tanzania, providing banking services to individuals, small to medium sized corporate clients, government services, large businesses and agriculture lending.

National Microfinance Bank PLC (NMB) ni miongoni mwa Benki kubwa za biashara hapa Tanzania, inayotoa huduma kwa wateja binafsi, wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa, serikalini na mikopo ya kilimo.

History

1997

NMB was established under the National Microfinance Bank Limited Incorporation Act of 1997, following the break-up of the old National Bank of Commerce, by an Act of Parliament. Three new entities were created at the time, namely: (a) NBC Holdings Limited (b) National Bank of Commerce (1997) Limited and (c) National Microfinance Bank Limited.

Initially NMB could only provide payment services as well as offer savings accounts, with limited lending capabilities, before becoming a fully-fledged universal retail bank.

Benki ilianzishwa kutokana na Sheria ya Bunge ya "National Microfinance Bank Limited" ya mwaka 1997, kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara kwa mujibu wa sheria ya Bunge. Taasisi tatu mpya ziliundwa wakati huo ambazo ni NBC Holding Corporation Ltd, National Bank of Commerce (1997) Limited na National Microfinance Bank Limited (NMB).

Mwanzoni NMB ilikuwa ikitoa huduma za malipo na akaunti za akiba pamoja na mikopo kwa kiwango kidogo.

1997

Historia

Subsequently, there was further divestiture in 2008 when the Tanzanian Government off loaded another 21% of its shareholding to the Tanzanian public through an Initial Public Offering (IPO). The listing of the bank's stock on the Dar es Salaam Stock Exchange has led to a diversified ownership structure.

2008

2005

In 2005, the Government of the United Republic of Tanzania privatized the bank when it sold part of its shareholding (49%) to a consortium led by the Coöperatieve Centrale Raiffeisen-Boerenleenbank B.A. ('Rabobank Group').

Mwaka 2005, Serikali ya Tanzania ilibinafsisha benki kwa kuuza asilimia arobaini na tisa (49%) ya hisa ilizomiliki kwa Ushirika uliokuwa ukiongozwa na Coöperatieve Centrale Raiffeisen-Boerenleenbank B.A. ('Rabobank Group').

2005

2008

Kwa mara nyingine, mwaka 2008 Serikali ya Tanzania ilipunguza tena asilimia ishirini na moja (21%) ya hisa zake kwenye benki kwa mara ya kwanza kwa umma wa Watanzania (Initial public offering).

Our Customers

NMB's customer base remains representative of Tanzania as a whole and includes government, civil servants, large corporate, SME's and MSE's, agriculture including small scale farmers, and microfinance institutions, as well as the Tanzanian public, both in rural and urban areas. NMB relies on its widespread distribution network to reach out to its customers and is one of the key players in improving financial inclusion in Tanzania.

Ownership

The total number of shareholders during the year 2013 is 29,119.

Our People

Our staff are also shareholders in NMB and together with their families have a direct interest and stake in the long term success of NMB.

Wateja wetu

Aina ya wateja wanaohudumiwa na NMB wana uwakilishi wa makundi yote ya Tanzania ikiwa ni pamoja na serikali, watumishi wa umma, mashirika makubwa, wateja wadogo na wa kati na wakubwa, wakulima wadogo na taasisi ndogo ndogo za kifedha, pamoja na umma wa Watanzania waishio vijijini na mijini. NMB inategemea mtandao wake mpana wa utoaji huduma katika kuwafikia wateja wake na ni moja ya taasisi zinazoongoza katika kuwawezesha Watanzania kupata huduma za kifedha.

Wafanyakazi

Wafanyakazi wetu ni wanahisa wa NMB, pamoja na familia zao wana masilahi ya moja kwa moja na ni sehemu ya mafanikio ya muda mrefu ya NMB.

Umiliki

Jumla ya wanahisa kwa mwaka 2013 inakadiriwa kufikia 29,119.

List of shareholders who individually own 0.5% or more shares as at 31 December 2013

Orodha ya Wanahisa wanaomiliki asilimia 0.5 au zaidi 31 Disemba, 2013

NAME OF SHAREHOLDER	NUMBER OF SHARES HELD	PERCENTAGE OF SHARES HELD
Coöperatieve Centrale Raiffeisen-Boerenleenbank B.A		
"Rabobank Nederland" (Rabobank)	174,500,000	34.9%
Treasury Registrar (Government of Tanzania)	158,901,800	31.8%
National Investment Company Limited (NICOL)	33,000,000	6.6%
Exim Bank (Tanzania) Limited	22,975,904	4.6%
Aunali F.Rajabali	11,588,882	2.3%
Sajjad F.Rajabali	11,435,526	2.3%
Standard Chartered Bank (T) Nominee Limited	10,150,249	2.0%
Standard Bank Plc	6,666,872	1.3%
Parastatal Pension Fund (PPF)	4,831,636	1.0%
National Social Security Fund (NSSF)	3,592,561	0.7%
TCCIA Investment Company Limited	2,611,886	0.5%

Founder Members

■ Rabobank Group

Rabobank is a full-range financial services provider operating on the basis of co-operative principles. Its origins are in the local loan co-operatives that were founded in the Netherlands more than 110 year ago by enterprising people who had virtually no access to the capital market. The local Rabobanks that evolved from this have a strong tradition in the agricultural sector and in small and medium-sized enterprises.

Rabobank is one of the leading banks in the Netherlands. Rabobank Group employs more than 58,000 people who serve approximately 10 million clients in 48 countries. In terms of Tier I capital, Rabobank Group ranks among the world's 25 largest financial institutions. Rabobank Group has the very high credit ratings, awarded by rating agencies Standard & Poor's, Moody's Investor Service and DBRS. For more information, please visit www.rabobank.com

Other founder members of the Rabobank Consortium are Exim Bank (Tanzania) Limited, National Investment Company Limited (NICOL) and TCCIA Investment Company Limited holding 11.7% of NMB shares.

■ Government of Tanzania

The Government of Tanzania holds 31.78% of the shares of NMB. It holds these shares through the Treasury Registrar in the Ministry of Finance.

Non Founder Members

Public shareholders hold 21.6% of the shares of NMB, with foreign investors also holding 3.3% of NMB shares, directly or as nominees.

Wanahisa Waanzilishi

■ Rabobank na Washirika wake

Rabobank inatoa huduma kamili za kifedha na inafuata dhana za vyama vya ushirika. Ilitokana na vikundi vya ushirika vya kukopeshana Uholanzi zaidi ya miaka 110 iliyopita vilivyojumuisha wajasiriamali ambao mwanzoni hawakupewa fursa ya kupata mitaji kutoka kwenye masoko ya mitaji. Rabobank iliyoungwa kutokana na misingi imara kwenye sekta ya kilimo na biashara ndogo ndogo na za kati.

Rabobank ni miongoni mwa mabanki yanayoongoza huko Uholanzi. Imejiri zaidi ya watu 58,000 ambao wanahudumia wateja wanaokadiriwa kufikia milioni 10 katika nchi 48. Kwa mtaji, Rabobank ni moja kati ya taasisi 25 kubwa zaidi za kifedha duniani, pia ina tathmini ya juu ya kukopesheka iliopewa na wakala wa tathmini Standard & Poor's, Moody Investor Services na DBRS. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea tovuti hii www.rabobank.com

Wanahisa wengine waanzalishi ni pamoja na benki ya Exim Tanzania, Kampuni ya Uwekezaji Tanzania (NICOL) na TCCIA Investment Company Limited.

■ Serikali ya Tanzania

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamiliki asilimia 31.78 ya hisa za NMB. Inamiliki hisa hizi kupitia kwa Msajili wa Hazina katika Wizara ya Fedha.

Wanahisa wasio waanzilishi

Umma wa Watanzania unamiliki asilimia 21.6 ya hisa za NMB na wawekezaji wa kigeni kupitia kwa mawakala pia wanamiliki asilimia 3.3 ya hisa za benki ya NMB.

5

Board of Directors | Bodi ya Wakurugenzi



Joseph Semboja
Board Chairman

Prof. Joseph Semboja is an acknowledged leader in the field of Development Economics, with extensive research experience in the areas of growth and poverty reduction. He holds a B.A and M.A from the University of Dar es Salaam, M.Sc and Ph.D. from the University of Illinois, Urbana-Champaign. He currently heads a leadership capacity building organization in the Institute of African Leadership for Sustainable Development (UONGOZI Institute).

Prof Joseph Semboja ni mtaalamu aliyebokea katika masuala ya uchumi, ana uzoefu mkubwa wa utafiti kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Ana shahada ya BA na MA kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, MSc na PhD kutoka Chuo Kikuu cha Illinois, Urbana – Champaign. Kwa sasa anaongoza taasisi ya kuimarisha uwezo wa viongozi inayojulikana kama UONGOZI Institute.

Lilian R. Komwihangiro is the Company Secretary and Legal Counsel of NMB. She holds a Bachelor of Laws degree and Master of Laws in commercial and business law, both from the University of Dar es Salaam. She also holds an MBA in Executive Management from the Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI) and is an Advocate of the High Court of Tanzania. Before joining NMB, she worked as a legal officer for Maajar, Rwechungura & Kameja Advocates, FK Law Chambers and as legal consultant at PricewaterhouseCoopers.

Lilian R. Komwihangiro ni Katibu wa Kampuni na Mwanasheria Mshauri wa NMB. Ana shahada ya Sheria na shahada ya juu ya Sheria katika nyanja ya Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ana shahada ya juu ya Usimamizi wa Biashara kutoka ESAMI. Pia ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kabla ya kujiunga na NMB alishawahi kufanya kazi kama Afisa Mwanasheria kwenye ofisi mbali mbali kama Maajar, Rwechungura & Kameja Advocates, FK Law Chambers na pia kama mwanasheria mshauri wa PricewaterhouseCoopers.



Lilian R. Komwihangiro
Company Secretary and Legal Counsel



Mike Laiser
Board Director

Mr. Mike Laiser is the former Director General of Small Industries Development Organisation (SIDO). Prior to SIDO, Mr. Laiser was an Executive Director of a UNDP funded income generation programme. He has over 25 years working experience in managing and consulting SME development in Tanzania and other SADC countries.

Bwana Mike Laiser aliwahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo (SIDO). Kabla ya SIDO Bwana Laizer aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Programu za msaada wa kukuza kipato za UNDP. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 25 katika kuongoza na kushauri wafanyabiashara wadogo na wa kati nchini Tanzania na katika nchi nyingine za SADC.

Mr. Jos van Lange is an Economist by profession and is currently the Chief Executive Officer of Rabo Real Estate Group, an international real estate company of Rabobank formed by the merger of several real estate companies. Prior to this role, Mr. van Lange was the Director of Retail Banking of Rabobank in the Netherlands.

Bwana Jos van Lange ni Mchumi kitaaluma na kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Makampuni ya Kimataifa ya Mali zisizohamishika ya Rabo, (Rabo Real Estate Group). Kampuni ya Kimataifa ya Mali zisizohamishika ya Rabobank awali iliungana na kampuni mbalimbali za mali zisizohamishika. Kabla ya kushika wadhifa huu, Bwana van Lange alikuwa Mkurugenzi wa kitengo cha huduma kwa wateja wadogo (Retail Banking) cha Rabobank ya Uholanzi.



Jos van Lange
Board Director



Anne Mbughuni
Board Director

Mrs. Anne Mbughuni is an Accountant by profession, registered with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) as a Certified Public Accountant. She holds an Advanced Diploma in Certified Accountancy, a Certified Public Accountant (CPA) professional degree and a Masters of Social Science in Accounting and Development Finance from the University of Birmingham, UK. She is currently the Director of Finance and Administration at the National Insurance Corporation of Tanzania Ltd.

Bi. Anne Mbughuni ni Mhasibu kitaaluma, amesajiliwa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) kama "Certified Public Accountant". Ana stahada ya juu ya Uhasibu, cheti cha juu cha kitaaluma katika uhasibu yaani CPA na shahada ya uzamili katika Sayansi ya Jamii katika Uhasibu na masuala ya Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza. Kwa sasa ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala katika Shirika la Bima la Taifa.

Mr. Protase Tehingisa is a specialist in corporate and investment law. He formerly worked as Secretary/Chief Legal Counsel of the East African Development Bank. Prior to that he worked as a State Attorney at the Attorney General's Chambers, and was also once the Corporation Counsel at the Tanzania Legal Corporation.

Bwana Protase Tehingisa ni mtalaamu wa sheria za uwekezaji wa makampuni. Amewahi kufanya kazi kama Katibu / Mwanasheria Mfawidhi katika Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB). Kabla ya hapo alikuwa Mwanasheria wa Serikali katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na pia alishawahi kuwa Mshauri katika Chama cha Wanasheria Tanzania.



Protase Tehingisa
Board Director



Margaret Ikongo
Board Director

Mrs Margaret Ikongo is a Chartered Insurer by profession. She was the Managing Director of the National Insurance Corporation for over 10 years. She has also served on the boards of different re insurance companies. She currently works as an independent insurance consultant.

Bi. Margaret Ikongo amesajiliwa kama "Chartered Insurer" katika taaluma ya Bima. Alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa zaidi ya miaka 10. Pia amewahi kuwa mkurugenzi wa bodi katika makampuni mbalimbali ya Bima. Kwa sasa ni mshauri wa kujitegemea katika masuala ya Bima.

Mr. Albert Jonkergouw has over 16 years' experience in retail and wholesale banking internationally and within Rabobank Netherlands. He holds two university degrees in Accounting & Auditing and is a member of NOREA (Netherlands Order of Registered IT Auditors) and the South African Institute of Professional Accountants (IPA). He is also a certified member of the Nyenrode Business University Non-Executive Director Board program. Mr. Jonkergouw is currently responsible for managing investments in Africa within Rabo Development.

Albert Jonkergouw kwa sasa anahusika na kusimamia vitega uchumi Afrika ndani ya Kitengo cha Maendeleo cha Benki ya Rabo na ana ujuzi wa miaka 16 wa shughuli za benki za wateja wadogo na wakubwa kimataifa ndani ya Benki ya Rabo ya Uholanzi. Kabla ya kujiunga na kitengo cha Maendeleo cha Benki ya Rabo, Bwana Jonkergouw alikuwa ni Kiongozi Mkuu Kimataifa wa Huduma za Ukaguzi katika Benki ya Rabo, na kabla ya kushikilia wadhifa huo alikuwa Afisa Mfawidhi wa Ukaguzi katika mabenki mbalimbali nchini Afrika ya Kusini.



Albert Jonkergouw
Board Director



William Mlaki
Board Director

Mr. William Mlaki has over 35 years of development banking experience. He was Managing Director of Tanzania Investment Bank for 13 years. He served on the boards of a number of companies and financial institutions within and outside Tanzania. He is currently an independent business consultant.

Bwana William Mlaki ana uzoefu wa zaidi ya miaka 35 katika shughuli za kibenki. Alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TIB kwa miaka 13. Pia amewahi kuwa mkurugenzi wa kwenye bodi za makampuni mbalimbali na taasisi za fedha hapa Tanzania na nje ya nchi. Kwa sasa ni mshauri wa kujitegemea katika masuala ya biashara.

NMB
Close to you



↓ TRY US

NMB Foreign Exchange Banking

Get all major foreign currencies accounts at competitive rates for your personal or business needs.

For more information,
walk in any of our branches



Experience the
**BEST BANK
IN TANZANIA**
Try us today!

www.nmbtz.com

6

Chairman's Report | Taarifa ya Mwenyekiti

It's a great pleasure for me to report to the shareholders and other stakeholders of National Microfinance Bank PLC (NMB) on the financial and operational results of the bank in 2013 which, once again, were very good and remain a solid foundation for sustainable success in the future, and for continued relevance to all our customers.

ina furaha kubwa kutoa taarifa ya fedha na matokeo ya utendaji wa benki kwa wanahisa na wadau wengine wa National Microfinance Bank PLC (NMB), kwa mwaka 2013, ambayo kwa mara nyingine, ni matokeo mazuri sana na yanabakia kama msingi imara kwa mafanikio endelevu kwa siku zijazo, na kwa benki kuendelea kuwa na umuhimu kwa wateja wetu.



Economic context

The bank has operated in the context of an improving economic environment, buoyed internationally by gradual recovery from the global economic crisis and by an increasingly favourable perception of international and local investors of the many and growing business opportunities on the African continent.

In Tanzania, the economy has continued growing at roughly 7% p.a., much in line with the previous 10 years, and among the more rapidly growing economies in the world.

Thanks to appropriate monetary and other policies by the Bank of Tanzania (BOT) and the Government of the United Republic of Tanzania (GOT), we have seen year on year inflation reduce from double digits to single digits, reaching as low as 5.6% in December 2013. This may have been aided by the stable Tanzania Shilling (TZS) exchange rate, particularly against the US Dollar, which has remained remarkably stable hovering between 1570 and 1630 during 2013.

Despite the country's high fiscal and current account deficits, there is an expectation that following the improvement in inflation indicators, a gradual reduction in market interest rates, both in the government securities may be in the cards, which may be followed by gradual reduction in interest rates on loans to the productive sector.

Financial Performance

Thanks to the resilient local economy and relatively buoyant interest rates, NMB has continued to do well in 2013. All key indicators point to solid growth, including loans (up 20% to TZS 1.6 trillion), deposits (up 13% to TZS 2.5 trillion). Once again NMB compared well to industry growth rates, implying that NMB continues to outperform its peers in key areas.

The bank's revenues grew strongly both on net interest income and non interest income lines.

Net interest income grew 18% to TZS 330 billion on the back of strong deposit growth which generated liquidity to fund loan growth and investment in government securities at roughly similar reinvestment rates as last year, while further improving the loan-to-deposit ratio from 59% to 63%.

Non interest income grew 18% to TZS 107 billion, with particularly good performance on the fees and commission line (up 17%), whereas trading income was somewhat disappointing, partially as a result of tightened regulatory environment on foreign exchange trading.

The bank's costs remained under control, growing 13.2% to TZS 225 billion. The ratio of staff costs to other operating costs remained stable at around 44%. The resulting cost to income ratio improved slightly from 55% to 57%.

Hali ya uchumi

Benki imefanya biashara katika mazingira ambapo uchumi umeboreka, ikisaidiwa kimataifa na ahueni ya taratibu kutoka kwenye mtikisiko wa kiuchumi duniani na mtazamo mzuri wa wawekezaji wa kimataifa na wa ndani kwa fursa nyingi na zinazoongezeka za biashara katika bara la Afrika.

Nchini Tanzania uchumi umeendelea kukua kwa takriban asilimia 7 kwa mwaka, kama ilivyokua katika miaka kumi iliyotangulia, na ikiwa moja ya nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi sana duniani.

Kutokana na sera nzuri za kifedha na sera nyingine za Benki Kuu ya Tanzania na Serikali, tumeshuhudia mwaka ambapo mfumuko wa bei umepungua kutoka tarakimu mbili hadi moja, kufikia kiwango cha chini cha asilimia 5.6 mwezi Disemba 2013. Hali hii itakuwa imesababishwa na uimara wa sarafu ya Tanzania (TZS), hasa dhidi ya dola ya Kimarekani, ambapo sarafu imebaki imara sana ikibadilishwa kwa kati ya dola 1570 na dola 1630 mwaka 2013.

Pamoja na pengo kubwa katika pato la nchi na nakisi kubwa ya bajeti, kupungua kwa mfumuko wa bei kunaleta mategemeo ya kushuka kwa taratibu kwa viwango vya riba katika soko na dhamana za serikali, ambako kunaweza kufuatiwa na kupungua kwa taratibu kwa viwango vya riba kwenye mikopo kwenye sekta ya uzalishaji.

Matokeo ya Kifedha

Kufuatia utulivu wa uchumi wa ndani na viwango vizuri vya riba, NMB imeendelea kufanya vizuri mwaka 2013. Viashiria vyote vinaonyesha ukuaji imara, ikiwemo mikopo (imeongezeka kwa 20% kufikia TZS 1.6 trilion) na amana (zimeongezeka kwa 13% hadi kufikia TZS 2.5 trilion). Kwa mara nyingine NMB iliendelea kufanya vizuri katika umiliki wa soko ikilinganishwa na mabanki mengine.

Mapato ya benki yaliongezeka sana kwa upande wa mapato halisi ya riba na mapato yasiyo ya riba.

Mapato halisi ya riba yalikua kwa asilimia 18 hadi TZS 330 bilioni kufuatia ongezeko kubwa la amana ambalo liliteta ukwasi uliowezesha kuongezeka kwa mikopo na uwekezaji kwenye dhamana za serikali kwa takribani sawa na viwango vya kuwekeza tena vya mwaka jana, sambamba na kuboresha uwiano wa mikopo na amana kutoka asilimia 59 hadi 63.

Mapato yasiyo ya riba yalikua kwa asilimia 18 kufikia TZS 107 bilioni, hususan kwa upande wa ada na kamisheni (ongezeko la asilimia 17), wakati mapato kutokana na biashara ya fedha yalikuwa si ya kuridhisha, hali ambayo kwa kiasi fulani ilitokana na ubanaji wa mazingira ya kisheria katika biashara ya fedha za kigeni.

Gharama za benki ziliweza kudhibitiwa, kukua kwa asilimia 13.2 hadi TZS 225 bilioni. Uwiano wa gharama za wafanyakazi kwa gharama nyingine za uendeshaji zilisimama kwenye asilimia 44. Uwiano wa gharama kwa mapato iliboreka kidogo kutoka asilimia 55 mpaka asilimia 57.

The non-performing loan (NPL) ratio remained stable at a low 2.6%, thanks to continued conservative write off and impairment decisions. The impairment coverage ratio on NPL's is now about 89%.

Overall, these favourable developments have contributed to strong improvement of the bank's Profit After Tax, up 37.5% to TZS 133.9 billion, while NMB's key performance indicators such as loan-to-deposit ratio (LDR) improved. The bank's return-on-average equity (ROAE) improved from 27% to 29%.

Share Price and Investor Relations

The bank's Net Asset Value (NAV) increased by 28% to TZS 456.6 billion. On a per share basis, the NAV per share increased from TZS 714 to TZS 913 per share, while earnings per share (EPS) increased from TZS 194.8 to TZS 267.81 per share.

Based on the favourable perceptions of African markets and NMB's relatively large share in the market capitalisation of the Dar Es Salaam Stock Exchange (DSE), investors were rewarded with an improved closing year-end price of TZS 2,620 per share, up 134% from TZS 1,120 in 2012. The closing share price implied a Price to book Value (PBV) multiple of 2.87, and and Price-Earnings ratio (PE) of 9.78.

Total shareholder return considerations included improvement in NAV per share, share price improvement and dividends paid.

Governance

The Board of Directors continues to subscribe to the highest standards of corporate governance, in applying where possible and best practice local, regional or global standards, and by initiating regular board and/or committee self-assessments and in endeavouring appropriate disclosures to stakeholders.

The Board of Directors also is closely involved in setting out the medium term strategy of the bank, which has been refined in the course of 2013.

As at December 2013, there remained one vacancy in the Board of Directors, and a search is ongoing to find a suitable candidate to fill this vacancy, for possible approval in a General Shareholders' Meeting of NMB.

Dividend Proposal

The board of Directors of NMB, in their meeting of 11th march 2014, recommended a dividend of TZS 90 per share, up 32.35% from the previous year.

The dividend proposals reflect the solid financial position of the bank, and its strong profitability. It also takes into account current regulatory guidelines, and anticipates on the possible further increased minimum regulatory capitalisation levels to be proclaimed by BOT, while complying with the bank's own prudent risk policies which

Uwiano mikopo isiyolipika imeendelea kuwa katika kiwango kinachoridhisha cha asilimia mbili (2.6%), tunashukuru kwa utaratibu mzuri wa kufuta madeni na kufanya maamuzi. Uwiano wa uwezo wa benki kukabiliana na mikopo isiyolipika ni 89%.

Kwa ujumla, maendeleo haya yamepelekea kuongezeka sana kwa faida kabla ya kodi, kukua kwa 37.5% hadi TZS 133.9 bilioni, wakati viashiria vikuu vya matokeo kama uwiano wa mikopo kwa amana (LDR) viliboreka. Wastani wa Mapato yatokanayo na wastani wa mali yatokanayo na hisa (ROAE) uliongezeka kutoka 27% hadi 29%

Bei ya Hisa na Mahusiano na Wawekezaji

Thamani halisi ya rasilimali za benki (NAV) iliongezeka kwa 28% mpaka TZS 456.6 bilioni. NAV kwa kila hisa iliongezeka kutoka TZS 714 hadi TZS 913 kwa kila hisa, wakati pato la hisa (EPS) liliongezeka kutoka TZS 194.8 hadi TZS 267.81.

Kufuatia mtizamo mzuri wa masoko ya Afrika na ukubwa wa NMB katika soko la mitaji la Dar es Salaam, wawekezaji walizawadiwa bei nzuri ya kufungia mwaka ya TZS 2,620 kwa kila hisa, ikiwa ni ongezeko la asilimia 134 kutoka TZS 1,120 ya mwaka 2012. Uwiano kati ya bei ya soko ya hisa na ya kufungia soko ilionyesha (PBV) wa 2.87, na uwiano kati ya bei ya hisa moja kwa mapato kwa hisa moja imefikia 9.78.

Pato la jumla la mwanahisa lilijumuisha ongezeko kwenye thamani halisi ya rasilimali za benki (NAV), ongezeko la bei ya hisa na gawio lililolipwa.

Utawala

Bodi ya Wakurugenzi inaendelea kutumia kanuni za utawala bora, katika kufuata viwango bora vya utendaji na pia bodi na/au kamati zake kuendelea kujipima mara kwa mara na kujaribu kujiweka karibu na wadau wake.

Bodi ya Wakurugenzi pia inahusika kwa karibu katika kutengeneza mikakati ya muda wa kati ya benki, ambayo ilipitiwa upya mwaka 2013.

Hadi Disemba 2013, kulikuwa na nafasi moja ya wazi kwenye Bodi ya Wakurugenzi, ambapo juhudi zinaendelea kumpata mtu anayefaa kujaza nafasi hiyo, ambaye atathibitishwa na Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa NMB.

Pendekezo la Gawio

Bodi ya Wakurugenzi wa NMB, katika mkutano wake uliofanyika tarehe 11 mwezi Machi mwaka 2014, ulipendekeza gawio la TZS 90 kwa hisa ambapo ni ongezeko la asilimia 32.35 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Pendekezo hili ni sambamba na ukuaji wa faida ya benki na sheria zilizopo zinazoongoza. Pia limezingatia kiwango cha kisheria kinachotakiwa kubaki ili kukuza mtaji ili kukabili mazingira yasiyotarajiwa, na kujiandaa na ongezeko la kiwango cha chini cha lazima cha mtaji kinachotarajiwa


have been adopted by the Board. It also takes into account the bank's investments in its future business strategies, including particularly its planned capital expenditures in IT and points of representation nationwide.

The proposed dividend at TZS 90 per share represents a dividend yield of some 3.4% based on the bank's December 2013 share price of TZS 2,620. The dividend pay out ratio would stand at 33.6% of the bank's net profit after tax.

Conclusion

The banks future prospects remain strong, based on the expected continued growth of the local economy, despite possible pressures around current and fiscal account deficits. A stable monetary policy combined with continued investment and private consumption which are expected to contribute to continued economic growth at 7% p.a. should bode well for the banking sector as a whole as well as for NMB. In the medium term the potential of agriculture and natural resources such as natural gas continue to beckon.

On behalf of the Board of Directors, I wish to thank management and staff for delivering another successful year, both financially and operationally, and of course all our stakeholders including Government of Tanzania, shareholders, and our customers for their support and loyalty to NMB.



Prof. Joseph Semboja
Chairman

kutangazwa na Benki Kuu ya Tanzania. Pia ni sambamba na sera za benki za uangalifu makini ambazo zimepitishwa na bodi. Pia imezingatia uwekezaji wa benki kufuatana na mikakati yake ya kibiashara kwa siku za baadae, ikiwemo uwekezaji kwenye mifumo ya TEHAMA na maeneo yake ya biashara nchini kote.

Pendekezo la gawio la TZS 90 kwa hisa, inawakilisha pato la hisa la asilimia 3.4 msingi wake ukiwa ni bei ya hisa ya TZS 2,620 ya Disemba 2013. Uwiano wa gawio utakuwa ni asilimia 33.6 ya faida halisi ya benki baada ya kodi.

Hitimisho

Matarajio ya baadaye ya benki ni mazuri, msingi wake ukiwa ni mategemeo kwamba uchumi wa nchi utaendelea kukua, licha ya shinikizo linalotokana na pengo la pato la nchi na nakisi ya bajeti. Sera thabiti ya fedha pamoja na kuendelea kwa uwekezaji na matumizi binafsi ambavyo vinategemewa kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi wa asilimia 7 kwa mwaka, ni viashiria vizuri kwa sekta ya fedha kwa ujumla na pia NMB. Katika muda wa kati uwezo wa sekta za kilimo na maliasili, kama vile gesi asilia unaendelea kuonesha mwelekeo mzuri.

Kwa niaba ya bodi ya wakurugenzi, ninapenda kushukuru uongozi wa benki na wafanyakazi kwa kuwa na mwaka mwingine wa mafanikio kifedha na kiutendaji na pia kuwashukuru wadau wetu wote ikijumuisha Serikali ya Tanzania, wanahisa wetu na wateja wetu kwa kuiunga mkono NMB.



Profesa Joseph Semboja
Mwenyekiti

7 Chief Executive Officer's Report | Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu

The year 2013 has been another remarkable year for NMB, continuing on its mission to provide affordable customer focused financial services to the Tanzanian community, through its extensive branch network, while realising sustainable benefits to all its stakeholders.

I'm pleased to report that NMB has had another year of record results, with Profit After Tax up 37% from TZS 97.4 billion to TZS 133.9 billion, and return on equity of 29%, with most business lines buoyed by a strong economic environment.

Mwaka 2013 ulikuwa mwaka mwingine wa mafanikio sana kwa NMB, kwani iliendeleza lengo lake la kutoa huduma za kibenki kwa gharama nafuu zenye kumlenga mteja wa jamii ya Kitanzania kupitia mtandao wake mpana wa matawi, huku ikitoa manufaa endelevu kwa wadau wake wote.

Ninayo furaha kutoa taarifa kwamba NMB ilikuwa na mwaka mwingine wa matokeo mazuri ya kifedha ambapo faida baada ya kodi imeongezeka kwa asilimia 37 kutoka TZS 97.4 bilioni mwaka uliopita kufikia TZS 133.9 bilioni mwaka 2013, rejesho kwenye faida za wanahisa la asilimia 29, hali iliyosaidiwa na mazingira yaliyoimarika ya kiuchumi.



We continually remind ourselves that as bankers, our primary responsibility is to remain relevant to our customers and it has therefore been equally gratifying to see continued improvements in our customer value propositions translated into increased business volumes across most segments and products.

Our consistency across the board performance was also rewarded for the first time in the bank's history by accolades from prestigious international publications such as Euromoney and The Banker, who selected NMB as "Best Bank in Tanzania 2013" and "Bank of the Year Tanzania 2013", respectively.

Economic Developments

The global economy has continued its gradual improvement, further supporting Tanzania's already very resilient economy which continued to grow at around 7% per year.

The local financial markets have remained stable, with headline inflation reducing to single digits, a stable exchange rate hovering between TZS 1570 and TZS 1630 to the US dollar for most of 2013, and reported year end international reserves of around USD 4.5 billion or approx. 4.5 months import cover.

Interest rates have remained relatively high on the back of a tight monetary policy stance from the Bank of Tanzania and in the context of a fairly high fiscal deficit and current account deficit. Yields on short term securities (less than one year) remained on average around 12 % p.a. (see figure below).

In the medium term, development of the natural gas sector in the coming years is expected to generate significant inflows from Foreign Direct Investments, but also outflows resulting from imports of capital goods, which may put further pressure on the structural current account deficit. The real impact of natural gas investments is not expected to start being felt before 2020 when the first gas is expected to start flowing.

Tunaendelea kujikumbusha kwamba kama benki, jukumu letu la msingi ni kuendelea kuwa muhimu kwa wateja wetu. Hivyo inafurahisha kuona jinsi tunavyoendelea kuboresha kwa adhama yetu ya jinsi ya kumpa mteja huduma ya thamani kunavyojitafiri katika kukua kwa biashara katika makundi na bidhaa mbalimbali.

Utendaji wetu mzuri katika vigezo mbalimbali pia umetambuliwa kwa mara ya kwanza katika historia ya benki kwa kutunukiwa tuzo kutoka majarida maarufu ya kimataifa ya Euromoney na The Banker, ambao waliichagua NMB kama "Benki bora nchini Tanzania 2013" na "Benki ya Mwaka Tanzania 2013" kwa mtiririko huo.

Maendeleo ya Kiuchumi

Uchumi wa dunia umeendelea kuimarika taratibu na hivyo kuusaidia zaidi uchumi wa Tanzania ulioweza kuhimili vizuri mabadiliko. Uchumi uliendelea kukua kwa asilimia 7 kwa mwaka.


Soko la fedha la ndani lilibaki imara, mfumuko wa bei ulishuka hadi kufikia tarakimu moja, bei ya kubadilisha shilingi kwa dola ilikuwa kati ya TZS 1570 na TZS 1630 kwa dola moja kwa kipindi kirefu cha mwaka 2013, na kiwango cha akiba ya fedha za kifizikia USD 4.5 bilioni au takriban kiwango cha kuagiza bidhaa kwa miezi 4.5 kutoka nje.

Viwango vya riba viliendelea kuwa vikubwa katika mazingira ya msimamo thabiti wa Benki Kuu katika kusimamia sera za fedha wakati ambapo kulikuwa na nakisi kubwa ya bajeti na katika urari wa biashara. Chumo kutoka kwenye dhamana za muda mfupi (zisizozidi mwaka mmoja) yalibakia kwenye wastani wa asilimia 12 kwa mwaka. (Tazama kielelezo hapo chini).

Katika muda wa kati, uendelezaji wa sekta ya gesi asilia unatarajiwa kuleta mapato kwa kiwango kikubwa katika miaka ijayo kutokana na Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje, lakini pia matumizi kutokana na gharama za uagizaji wa bidhaa za mitaji, ambayo inaweza kuweka shinikizo zaidi kwenye pengo la pato la taifa. Matunda halisi ya uwekezaji katika gesi asilia hayategemewi kuanza kuonekana kabla ya mwaka 2020 wakati gesi ya kwanza inatarajiwa kuanza kuzalishwa.

Figure 1: TZS vs USD exchange rate trend


Kielelezo 1: Mwelekeo wa viwango vya TZS vs USD




Source: Bank of Tanzania website.

Figure II (i): Treasury Bills Yields


Kielelezo II (i): Chumo kutokana na Hawala za Serikali

**Figure II (ii): Treasury Bonds Yields**

Kielelezo II (ii): Chumo Kutokana na Dhamana za Serikali

**Figure II (iii): Headline inflation rate**

Kielelezo II (iii): Mfumuko wa Bei



However there are good hopes that until then the economy will continue growing at least at 7% p.a., despite continued high fiscal and current account deficits, powered by strong domestic consumption.

Market Developments

The Tanzanian banking market now has as many as 52 licensed banks (50 in 2012), who together operated 609 branches (of which NMB owns 153, or 25%), and total assets of TZS 17.9 trillion (of which NMB represent TZS 3.2 trillion or 18%).

According to data published by banks pursuant to section 32 (3) of the Banking and Financial Institutions Act, the markets have developed as follows:

Table I: Market Growth 2013

	TOTAL MARKET	TOP 8 BANKS	NMB PLC
Deposit growth	8%	9%	13%
Advances growth	15%	11%	20%
Total Income growth	15%	13%	18%
Operating Cost/			
Total Income	73%	73%	53%
Loan/Deposit Ratio	68%	62%	63%

According to these same published data, the NMB's market shares evolved as follows:

Table II: NMB PLC Market share

	2011	2012	2013
Deposits	16%	19%	20%
Advances	16%	17%	18%
Total Income	23%	25%	25%
Profit after Tax	31%	38%	48%

Financial Results

NMB was able to continue its customer deposit generation in 2013 on the back of the successful "Jisevie" and "Try Us" customer campaigns. It was gratifying to see these campaigns translate into full year deposit growth of some 13%, roughly at market. The increased liquidity was allocated to a growing loans and advances book (up 20%) and to government securities.

This deposit generation and changes in the mix in allocation to loans and advances and securities resulted in an improvement of the loan-to-deposit ratio to some 63%. Total interest income benefited from continued relatively high interest rates both on the lending and investment side, coupled with good lending and investments volume growth. As a result, net interest income grew by a respectable 18% year-on-year.

Hata hivyo kuna matumaini makubwa kwamba mpaka wakati huo uchumi utakuwa ukiendelea kukua kwa kasi ya takriban asilimia 7 kwa mwaka, licha ya kuendelea kwa mazingira ya nakisi kubwa ya kifedha na pengo katika pato la taifa zinazosababishwa na matumizi makubwa ya ndani.

Maendeleo ya Soko

Soko la benki nchini kwa sasa lina jumla ya mabanki 52 yenye leseni (50 yalikuwepo mwaka 2012), ambayo yote kwa pamoja yana matawi 609 (ambapo kati ya hayo NMB ina matawi 153 au asilimia 25) na rasilimali za jumla ya TZS 17.9 trilion (ambapo kati ya hizo zile za NMB zina thamani ya TZS 3.2 trilion au asilimia 18).

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na mabanki yote kwa mujibu wa kifungu cha 32 (3) cha Sheria za Mabanki na Taasisi za Fedha, kuna ongezeko katika soko kama ifuatavyo:

Jedwali I: Ukuaji wa Soko 2013

	SOKO KWA UJUMLA	MABENKI 8 MAKUBWA	NMB PLC
Ukuaji wa Amana	8%	9%	13%
Ukuaji wa Mikopo	15%	11%	20%
Ukuaji wa Mapato ya jumla	15%	13%	18%
Gharama za Uendeshaji/Mapato ya jumla	73%	73%	53%
Uwiano wa Mikopo/Amana	68%	62%	63%

Kwa mujibu wa takwimu hizi, soko la NMB liliongezeka kama ifuatavyo:

Jedwali II: Ukubwa wa Soko la NMB PLC

	2011	2012	2013
Amana	16%	19%	20%
Mikopo	16%	17%	18%
Mapato	23%	25%	25%
Faida Baada ya Kodi	31%	38%	48%

Matokeo ya Kifedha

NMB iliendelea kukuza amana zake mwaka 2013 kufuatia kampeni zilizofanikiwa za "Jisevie" na "Try Us". Inafurahisha kuona kwamba kampeni hizi zimepelekea ukuaji wa amana kwa takriban asilimia 13 kwa mwaka mzima sambamba na ukuaji wa soko. Ongezeko la ukwasi lilisababishwa na ukuaji katika utoaji mikopo (ongezeko la asilimia 20) na dhamana za serikali.

Upatikanaji huu wa amana na mabadiliko katika mchanganyiko wa utoaji mikopo na dhamana uliboresha uwiano wa mikopo-kwa-amana hadi asilimia 63. Mapato ya jumla yatokanayo na riba yalisaidiwa na kuendelea kuwepo kwa riba kubwa katika upande wa

Non-funded income grew by 18% to TZS 107 billion, on the back of higher customer transactional volumes generating increased commissions, while foreign exchange trading income remained somewhat disappointing despite higher customer volumes as a result of low market volatility and tighter regulatory environment.

Accordingly, total revenues grew by about 18% to TZS 422.2 billion.

On the expense side, total expenses growth rate at 13% remained well below the revenue growth rate of 18%, which translated in a cost to income ratio of 53%. Staff costs represent about 44% of total expenses.

With regards to the risk profile of NMB's lending activities we are pleased to report another year of fairly low NPL's at around 2.6%. This is as a consequence of NMB's conservative lending appetite and impairment and write off policies. Cumulative impairments as at the end of the year amounted to TZS 38.1 billion, or 2% of the year end loan book, and write offs represented 1%.

Overall the bank's Profit After Tax (PAT) increased by a respectable 37% to TZS 133.9 billion.

The bank's key efficiency ratios remained stable or improved viz. the cost-to-income ratio which improved from 55% to 53%, and the loan-to-deposit ratio which improved from 59% to 63%, though remaining well below the regulatory maximum of 80%.

The bank's return on equity improved from 27% to 29% while the core capital of the bank grew to TZS 421.8 billion, resulting in a capital adequacy ratio of 22% (before appropriation of profits), also well above the increased regulatory minimum of 12%.

In generating these strong results, it is also useful to share how the value created was allocated between NMB's key stakeholders:

- To Government of Tanzania (GOT) (in the form of income taxes, PAYE, SDL etc...) TZS 79.6 billion.
- To shareholders (incl. GOT) and other providers of capital (in the form of dividend TZS 34 billion).
- To employees (in the form of salaries and benefits) TZS 99.7 billion.
- To other stakeholders (in the form of sponsorships, Public Relations donations etc) TZS 1.05 billion.

From these very encouraging and strong results, it becomes apparent that there is a balanced allocation of value created, with a large proportion of the value created by NMB reverting back to Government of Tanzania.

Business Developments

NMB key business lines include Wholesale Banking, Retail banking and Treasury, whose chosen customers benefit of NMB's growing range of transactional-, lending-, savings- or investment-, and foreign exchange solutions.

utoaji mikopo na uwekezaji, sambamba na ongezeko la mikopo na uwekezaji. Kwa hiyo, mapato halisi yatokanayo na riba yaliongezeka kwa kiwango kizuri cha asilimia 18 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Mapato yasiyotokana na riba yalikua kwa asilimia 18 kufikia TZS 107 bilioni, kufuatia miamala mikubwa zaidi iliyoongeza mapato kutokana na kamisheni. Mapato yaliyotokana na biashara ya fedha za kigeni hayakuwa ya kuridhisha licha ya idadi kubwa ya wateja, hii ilitokana na mabadiliko madogo ya bei katika soko na mazingira ya kisheria yenye udhibiti mkali zaidi.

Kwa hiyo, mapato kwa ujumla yaliongezeka kwa asilimia 18 kufikia TZS 422.2 bilioni.

Kwa upande mwingine, ukuaji wa jumla wa matumizi wa asilimia 13, ulikuwa chini ya ukuaji wa mapato wa asilimia 18, iliyoepesha uwiano wa asilimia 53 wa matumizi kwa mapato katika mwaka. Gharama za wafanyakazi zilikuwa ni asilimia 44 ya matumizi yote.

Kwa upande wa shughuli za mikopo, inafurahisha kuona benki iliendelea kuwa na uwiano mdogo wa mikopo chechefu (inayoweza kutolipika) wa asilimia 2.6. Uwiano huu mdogo wa mikopo chechefu unatokana na msimamo thabiti wa kudhibiti hasara itokanayo na mikopo. Hasara kutokana na mikopo isiyolipika kwa mwaka ni TZS 38.1 bilioni, au asilimia 2 ya mikopo yote, na mikopo iliyofutwa ni 1%.

Kwa ujumla, Faida ya benki Baada ya Kodi iliongezeka kwa kiwango kizuri cha asilimia 37 kufikia TZS 133.9 bilioni.

Vilevile, uwiano wa vigezo vya ufanisi vimebaki vilevile au kuongezeka Uwiano wa gharama na mapato uliboreka kutoka asilimia 55 hadi asilimia 53 na uwiano wa mikopo na amana uliboreka kutoka asilimia 59 mpaka asilimia 63, licha ya kuwa chini ya kiwango cha juu cha sheria za benki cha asilimia 80.

Pato linalotokana na mtaji lilikua kutoka asilimia 27 hadi asilimia 29, wakati mtaji wa msingi wa benki ulikua kufikia TZS 421.8 bilioni, na kuwezesha kiwango toshelezi cha mtaji cha asilimia 22 (kabla ya kuondoa kodi) kikiwa juu ya kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 12 kwa mujibu wa sheria za benki.

Katika kuangalia matokeo ya kifedha ya benki, ni muhimu kuangalia jinsi thamani iliyozalishwa ilivyogawanywa kwa wadau wa msingi wa NMB.

- Kwa Serikali ya Tanzania (ikihusisha kodi ya mapato, PAYE, SDL n.k...) TZS 79.6 bilioni.
- Kwa wanahisa (ikiwemo serikali) na watoa mtaji (ikihusisha gawio TZS 34 bilioni).
- Kwa wafanyakazi (ikihusisha mishahara na stahili) TZS 99.7 bilioni.
- Kwa wadau wengine (kupitia udamini, uhusiano wa jamii, misaada n.k.) TZS 1.05 bilioni.

Key business lines are supported by divisions such as ICT and Operations, Human Resources, Finance. Oversight and control is provided by divisions such as Risk, Internal audit.

- Our **Wholesale Banking** business line includes Corporate Banking (large corporate customers and parastatals), Government Banking (central and local government), Institutional Banking (insurance, pension funds, NGO's, government agencies etc...) and Agribusiness (crop financing), supported by a specialised Transactional Services team.

- Generally the team has shown good progress in further improving the mix of lending and non lending business, including foreign exchange, trade finance and payments and collections. The Wholesale banking division loan book, including agriculture, represents approx. 25% of the banks total loans. With over 153 branches nationwide and a full range of electronic transactional solutions for payments and collections, we have a compelling offering, with an increasing number of the country's leading Corporates and Institutions considering NMB as their core bankers. We are also making inroads in facilitating some of the country's oil importers and are seeing encouraging trade finance volume growth.

- Our Government business has remained stable. NMB won six out of the seven geographic Lots tendered by GOT, and we are also making good progress in developing new business opportunities with Government outside the narrow definition of the Banking Services Tender. There is a continuing effort to improve service levels and increase straight through processing for all customers, including GOT.

- Our Agriculture team continues to provide financing to hundreds of Agricultural Marketing Cooperatives (Amcos), to whom we provide input finance, warehouse receipt finance and other financing, despite challenging regulatory circumstances, a fragmented sector and regular interference in the markets. The team also finances larger commercial and emerging farmers, and provides financing to outgrowers of selected industrial farming complexes.

- Our **Retail Banking** business lines includes Personal Banking (including civil servants) and M-SME banking, to whom we provide the full range of lending, transactional and savings solutions, supported by continued investments in technologies.

- Loans to individuals (mostly salary backed loans, based on deduction codes) continued to grow strongly at about 24%, with the loan portfolio representing some 54% of total loans and advances. Current and savings account balances owed to individuals also grew well at about 14% on the back of our Jisevie and Try Us campaigns. These campaigns also resulted in increased transactional volumes, which supported our fees and commissions growth.

Kufuatia matokeo haya mazuri na ya kufurahisha, ni wazi kwamba kuna uwiano mzuri katika mgawo wa thamani iliyozalishwa, huku kiasi kikubwa cha thamani iliyozalishwa na NMB kikirudi kwa Serikali ya Tanzania.

Maendeleo ya Biashara

Maeneo makuu ya biashara ya NMB ni Biashara ya Jumla , Wateja wa Reja reja na Hazina, ambapo wateja wanafaidika na ongezeko la aina ya ufumbuzi wa miamala na huduma na bidhaa za mikopo, akiba, uwekezaji na fedha za kigeni.

Maeneo haya makuu ya biashara yanasaidiwa na vitengo kama TEHAMA na Operesheni, Raslimaliwatu, Fedha. Udhibiti wa Hasara na Ukaguzi wa Hesabu.

- Kitengo chetu cha **Biashara ya Jumla** kinalenga kwenye mahitaji ya kifedha ya wateja wakubwa na makampuni makubwa, serikali (serikali kuu, serikali mitaa na taasisi zake), taasisi nyingine (bima, mifuko ya pensheni, NGO's, wakala wa serikali n.k) na biashara ya kilimo (kuwezesha kilimo cha mazao), kikiwa na timu mahsusi ya huduma.

- Kwa ujumla timu imefanya kazi nzuri katika kuboresha mchanganyiko wa biashara ya mikopo na isiyo ya mikopo, ikiwamo biashara ya fedha za kigeni, biashara za fedha na malipo na makusanyo. Mikopo iliyotolewa na kitengo cha biashara ya jumla, ikiwemo ya kilimo, ni takriban asilimia 25 ya mikopo yote iliyotolewa na benki. Ikiwa na mtandao wa matawi 153 nchini kote na aina mbalimbali za ufumbuzi wa miamala ya kielektroniki kwa malipo na makusanyo, tuna mvuto mkubwa, huku makapuni makubwa na taasisi zikiitumia NMB kama benki yao ya msingi. Tumeingia pia katika kuwezesha baadhi ya wafanyabiashara waagizaji wa mafuta nchini na tunaona mafanikio kwenye ukuaji wa biashara.

- Biashara yetu na serikali imebaki imara. NMB ilishinda mafungu sita ya kijiografia kati ya yale yaliyotolewa na serikali kwa njia ya zabuni. Tunapata mafanikio pia katika kuongeza fursa za kibiashara kati yetu na serikali nje ya tafsiri finyu ya Zabuni za Huduma za Kibenki. Kuna jitihada zinazoendelea kuboresha na kuongeza viwango vya huduma kwa wateja wote, ikiwemo serikali.

- Kitengo chetu cha kilimo kinaendelea kutoa mikopo kwa mamia ya Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Kilimo (Amcos). Tunatoa mikopo ya pembejeo, stakabadhi za mazao ghalani na mikopo ya aina nyingine, licha ya sekta hii kuwa na mazingira magumu ya kisheria katika udhibiti wa fedha. Timu pia inatoa mikopo kwa wakulima wakubwa wa kibiashara na wakulima wa mkataba kwenye baadhi ya maeneo ya kilimo kwa ajili ya viwanda.

- **Biashara yetu kwa wateja wa reja reja** inajumuisha Wateja Binafsi (wakiwemo watumishi wa umma) na wajasiriamali na wa Kati, ambao tunawapa huduma zote za mikopo, ufumbuzi wa miamala na akiba, ikiimarishwa na uwekezaji unaoendelea katika teknolojia.

- Loans and advances to Micro, Small and Medium Enterprises (M-SME's) continued also to grow well at around 15%, representing about 20% of total loans and advances. We are supporting our MSME customers through Reginal Business Clubs.
- Further customer service improvements were achieved in a number of areas, with a clear NMB Service Commitment towards our customers.
- Our new remote instant account opening offering was launched in 2013 under the Chap Chap brand. The Chap Chap account is a low cost entry level account, without monthly fees and powered by NMB Mobile, an ATM card and biometrics. It is sold offsite (outside our branches).
- A key constraint to formal financial inclusion remains the high KYC requirements imposed by the regulatory environment, which are prohibitive in cost and complexity to a large proportion of the unbanked population.
- On the Distribution side, our branch network increased from 147 to 153 branches, of which 136 are in rural areas, and 17 are in Dar Es Salaam. We have also continued to expand our network of Business Centres, targeted at large corporates, SME's and Government. These are located in Arusha city, Mwanza city and Dar es Salaam. A major project is underway to upgrade our branches look and feel, for the benefit of our staff and customers, with over 100 branches slated for renovation.

We have continued to enhance our self-service channels. NMB operated 485 ATM's at year end and in 2013 we entered into a cooperation with Vodacom, a Mobile Network Operator (MNO), allowing NMB Mobile customers to transact directly to and from their M-Pesa mobile payment platform. This effectively expanded the bank's physical distribution with another 40,000 additional cash-in/cash-out points operated by M-Pesa agents.

The customer take up has been impressive, also contributing significantly to the bank's fees and commissions lines. A similar integration arrangement with Tigo, another MNO, is also in the cards.

On the other side, the banking industry continues to face challenges, as a result of a lack of level playing field between banks and Mobile Network Operators (MNO's), with bank customers subjected to much tighter Know Your Customer (KYC) and Anti Money Laundering (AML) requirements than the MNO's.

- Our **Treasury** Business line includes TZS money markets and foreign exchange trading.

The money market activities have benefited from increased deposit generation which was partially re-invested in securities. Higher volumes, improved short term and longer term funding and gapping

- Mikopo kwa watu binafsi (hasa mikopo ambayo marejesho yanakatwa kwenye mshahara) iliendelea kuongezeka kwa kasi ya takriban asilimia 24, huku mikopo iliyotolewa kwenye kundi hili ikiwa ni asilimia 54 ya jumla ya mikopo yote. Akiba kwenye akaunti za hundi na akiba za watu binafsi zilikuwa kwa takriban asilimia 14 kutokana na kampeni za 'Jisevie' na 'Try Us'. Kampeni hizi pia ziliongeza ukubwa wa miamala, na hivyo kuongeza makusanyo ya ada na kamisheni.
- Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo Wadogo na wa Kati (M-SME) iliendelea kukua vizuri kwa takriban asilimia 15 ikiwakilisha asilimia 20 ya mikopo yote. Tunahudumia wateja hawa kwa kupitia klabu za biashara za kanda.
- Maboresho katika huduma kwa wateja yalikuwepo kwenye maeneo mengi mengine, yakifanywa kwa Dhamira dhahiri ya NMB kuwahudumia vizuri wateja wake.
- Huduma yetu ya kufungua akaunti nje ya matawi ya benki ilizinduliwa mwaka 2013, kwa chapa ya Chap Chap. Akaunti hii hufunguliwa kwa kiasi kidogo cha fedha, haina ada za kila mwezi, na inaendeshwa kwa NMB Mobile, kadi ya ATM na biometriki.
- Kikwazo kikubwa katika kujiunga na huduma za kifedha kinabakia kuwa ni matakwa makubwa ya Mjue Mteja Wako (KYC) yaliyowekwa kisheria, ambayo hayavutii kutokana na gharama na ugumu kwa wananchi wengi ambao hawatumii huduma za kibenki.
- Kwa upande wa mtandao, idadi ya matawi yetu iliongezeka kutoka 147 hadi 153 ambapo matawi 136 yapo katika maeneo ya vijijini, na 17 yapo Dar es Salaam.

Tumeendelea pia kupanua mtandao wetu wa Vituo vya Biashara, vinavyolenga makampuni makubwa, Wajasiriamali Wadogo na wa Kati na Serikali. Haya yapo Arusha, Mwanza na Dar es Salaam. Mradi mkubwa unaendelea kuboresha muonekano wa majengo ya matawi yetu, kwa faida ya wafanyakazi wetu na wateja, ambapo matawi yetu 100 yatafanyiwa maboresho.

Tumeendelea kuboresha njia za huduma zinazomwezesha mteja kujihudumia mwenyewe. NMB ilikuwa na ATM 485 ilipofika mwishoni mwa mwaka.

Mwaka 2013 tulifikia makubaliano na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom, kuruhusu wateja wa NMB wanaotumia huduma ya simu kufanya miamala ya kutoa na kuweka fedha moja kwa moja kwenye M-Pesa. Hatua hii ilipanua kwa kiasi kikubwa mtandao wa NMB kwa kuwa na sehemu 40,000 zaidi za kuweka na kutoa fedha zinazoendeshwa na mawakala wa M-Pesa. Wateja wengi wanatumia huduma hii, na hivyo inachangia sana kwenye mapato ya benki yanayotokana na ada mbalimbali na kamisheni. Mpango kama huo uko mbioni ili kushirikiana na kampuni nyingine ya huduma za simu za mkononi ya Tigo.

Kwa upande mwingine, tasnia ya benki inaendelea kukabiliwa na changamoto, kutokana na kukosekana

initiatives resulted in strong interest income growth. There was an increase in interest expenses partially on the back of two large funding deals from Nederlandse Financieringsmaatschappij voor Ontwikkelingslanden N.V. (FMO) and European Investment Bank (EIB) respectively. Both facilities allowed NMB to improve the tenor mismatch between assets and liabilities, with the increased funding cost for longer term funding deemed appropriate despite the bank's otherwise significant excess liquidity.

On the foreign exchange side, revenues were somewhat disappointing despite strong growth in customer foreign exchange volumes. This is largely as a result of lower market volatility and increased regulatory oversight. The growth of customer foreign exchange volumes is also as a result of joint efforts with the Wholesale Banking teams to achieve more balanced customer relationships by enhancing payments, collections, trade finance and foreign exchange flows. Also we are seeing good opportunities for Retail foreign exchange, which is coming off a very low base. A new Treasury Management System has been procured and is in the final User Acceptance Testing phase before being fully implemented in early 2014.

- Our **ICT and Operations** division is tasked to build and operate the required infrastructure to facilitate and process all customer transactions centrally and in the branches.

kwa ushindani ulio sawa kati ya mabanki na makampuni ya simu, ambapo wateja wa benki wanabanwa zaidi na mahitaji ya Mjue Mteja Wako (KYC) na Sheria ya Fedha Haramu (AML) kuliko wale wa makampuni ya simu.

- Kitengo chetu cha Hazina** kinajumuisha masoko ya fedha za Tanzania (TZS) na biashara ya fedha za kigeni. Shughuli za masoko ya fedha zimenufaika na kukua kwa amana ambazo kwa kiasi fulani ziliwekezwa kwenye dhamana. Kuongezeka kwa biashara, kuongezeka kwa mikopo ya muda mfupi na muda mrefu na hatua za kuziba pengo kati ya fedha zilizopo na zinazohitajika kulipelekea kukua kwa mapato ya benki yatoanayo na riba. Kulikuwa na ongezeko katika gharama za kulipia riba kutokana na mikopo mikubwa miwili kutoka Nederlandse Financieringsmaatschappij voor Ontwikkelingslanden N.V. (FMO) na European Investment Bank (EIB). Mikopo yote hii miwili imeiwezesha NMB kuboresha mizania yake na hasa uwiano kati ya rasilimali na madeni.
- Kwa upande wa biashara ya fedha za kigeni, mapato hayakuwa ya kuridhisha licha ya kuongezeka kwa ubadilishaji wa fedha za kigeni uliofanywa na wateja. Hii ilisababishwa zaidi na mabadiliko madogo ya bei katika soko na udhibiti mkali wa bei kwenye soko la fedha za kigeni. Ongezeko la ubadilishaji fedha uliofanywa na wateja pia ni matokeo ya juhudi za pamoja za timu ya Hazina na ile ya Biashara ya Jumla kuboresha uwiano wa mahusiano na wateja kwa kuimarisha mtiririko wa malipo, makusanyo, biashara ya fedha na fedha za kigeni. Pia tunaona fursa nzuri kwa biashara ya reja

Table III: new branches opened / Jedwali III: matawi mapya yaliyofunguliwa

NEW BRANCHES OPENED/MATAWI MAPYA YALIYOFUNGULIWA	2011	2012	2013
Number of branches at start of the year	139	142	147
Namba ya matawi mwanzoni mwa mwaka			
Branches opened			
PPF - Mwanza	1		
Nanyumbu Mtwara	1		
Arusha Palace Business Centre	1		
Mbezi - Dar es Salaam		1	
Maktaba - Dar es Salaam		1	
Tegeta - Dar es Salaam		1	
UDOM - Dodoma		1	
Kurasini - Dar es Salaam		1	
Congo Street - Dar es Salaam			1
Himo - Kilimanjaro			1
Buzuruga - Mwanza			1
Ubungo - Dar es Salaam			1
USA River - Arusha			1
Sinza - Dar es Salaam			1
Total opened during the year	3	5	6
Jumla ya matawi yaliyofunguliwa kwa mwaka			
Number of branches at the end of the year	142	147	153
Namba ya matawi mwishoni mwa mwaka			

- In late 2011 NMB migrated to a new state of the art Core Banking System (CBS). The CBS is showing solid performance, processing close to 5 million transactions per month. The CBS has remained stable in 2013 with no major incidents impacting our customers. Efforts are underway to continually upgrade the operating environment, including by way of Straight Through Processing, further improving the ratio of electronic to manually initiated transactions.
- Ancillary applications to support ATM network, NMB Mobile, MNO integration solutions or otherwise have also generally shown good and improving uptimes.
- Fraud risks, including ATM card skimming, have remained limited thanks to adequate preventive measures and strong follow up in cooperation with the judicial authorities.
- A new project is underway to ensure the ICT environment is further upgraded, not only in terms of hardware and software, but also in terms of governance standards and other best practices. This is a necessity in light of the expected continued investments in upgraded or new electronic and self service solutions to be developed for our customers, including large corporate or institutional customers.
- Our **Human Resources** team is tasked to ensure we have the right people in the right jobs, at head office and over 153 branches.
- In the course of 2013 we continued in our efforts to improve the working environment for our close to 2,850 staff members. Staff engagement, direct, through union representatives, through our Employee Opinion survey, or otherwise yielded new opportunities to that effect. A number of initiatives, including further strengthening of performance management, new training and certification programmes, review of rewards and benefits, medical coverage and staff welfare programmes contributed to the further improvement of the work environment. The ongoing branch refurbishment programme is also designed to upgrade our employees work space.
- Our **Finance** division is tasked to produce reliable financials for accounting and reporting purposes, but also to provide the various divisions with the required numbers they can use in driving their businesses.
- In the course of 2013 the finance team was recognised by the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) for the Best Presented Financial Statements by a financial institution in Tanzania. And once again, NMB was recognised by Tanzania Revenue Authority (TRA) as one of the largest and most compliant tax payers. Efforts are underway to continue improving the bank's Management Information Systems (MIS) in support of the various business divisions strategies.

- reja ya fedha za kigeni, inayokua kutoka kwenye msingi mdogo.
- Mfumo mpya wa kusimamia Hazina umenunuliwa na uko kwenye hatua za mwisho za majaribio ya kukubaliwa na mtumiaji kabla haujaanza kutumika rasmi mapema mwaka 2014.
 - **Kitengo chetu cha TEHAMA** na Operesheni kimepewa jukumu la kujenga na kuendesha miundombinu ya kuchakata miamala yote ya wateja kupitia makao makuu na kwenye matawi.
 - Mwishoni mwa mwaka 2011, NMB ilianza kutumia mfumo wa kisasa wa uendesaji wa benki kwa kutumia kompyuta. Mfumo huu ni thabiti na unachakata miamala takriban milioni 5 kwa mwezi. Mfumo huu ulifanya kazi vizuri mwaka 2013 bila matukio yoyote makubwa ambayo yangukuwa na athari kwa wateja. Juhudi zinafanywa kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji, ikiwemo kutumia utaratibu wa moja kwa moja unaojulikana kama "Straight Through Processing", na hivyo kuboresha uwiano kati ya miamala ya kielektroniki na ile isiyotumia mashine.
 - Vifaa vya ziada kwa ajili ya kusaidia utendaji wa mtandao wa ATM, "NMB Mobile" na muingiliano wa mfumo ya benki na ile ya makampuni ya simu za mkononi kwa ujumla vimeonesha kuboresha utendaji.
 - Vitendo vya uhalifu, ikiwemo wizi wa taarifa kutoka kwenye kadi za ATM, vimehibitiwa kutokana na hatua za kutosha za kinga na ufuatiliaji wa karibu unaofanywa kwa kushirikiana na vyombo vya sheria.
 - Kuna mradi mpya unaolenga kuboreshwa zaidi kwa mazingira ya TEHAMA, siyo tu kwa mashine na programu, lakini pia kwa viwango vya utawala bora na utendaji bora. Hii ni muhimu kwa sababu tunategemea kuendelea kuwekeza katika uboreshaji au uwekaji wa mifumo mipya ya kielektroniki na mifumo inayomwezesha mteja kujihudumia mwenyewe, itakayowekwa kwa ajili ya wateja wetu, yakiwemo makampuni makubwa na taasisi.
 - Timu yetu ya **Rasilimali watu** imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba nafasi za kazi zinajazwa na wale tu wenye sifa za kufanya kazi hizo iwe makao makuu au kwenye matawi yote 153.
 - Mwaka 2013 tuliendelea na juhudi zetu za kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wetu wanaofikia 2,850. Mahusiano na wafanyakazi, moja kwa moja au kwa kupitia uwakilishi wa vyama vya wafanyakazi, kupitia utafiti wa kupata Maoni ya Wafanyakazi, na namna nyingine, kulileta fursa zilizosaidia kuboresha mazingira ya kazi. Hatua mbalimbali zikiwemo kuimarisha jinsi ya Kupima Utendaji (Performance Management), programu za mafunzo kupitia upya taratibu za utoaji marupurupu ya ziada na stahili, matibabu na programu za ustawi wa wafanyakazi zilichangia kuboresha zaidi mazingira ya kazi. Programu

- The **Risk** function provides independent oversight and control on the bank's operational, credit, market, compliance and other risks.

At the most visible levels our conservative risk standards have translated into continued low NPL levels as well as high NPL coverage ratios. But behind these numbers lie a series of significant initiatives to keep improving the entire risk management environment. On the resourcing side we have strengthened our Market risk team and created a Special Asset Management (SAM) team.

On the loan management side, we are developing new credit scoring practices, and improving our efficiency by way of a central loan processing unit. AML and KYC remain centre stage and we are well underway to achieve full compliance to new and increased KYC standards promulgated by GoT, supported by new AML systems designed to improve detection of suspicious transactions. At the highest level, the bank has embarked on a multi-year Enterprise Risk Management (ERM) project to fully embed risk awareness and management as a core competency at all levels in the organisation.

- The **Internal Audit** (IA) function reports functionally to the Board of Directors through the Board Audit, Risk and Compliance Committee (BARCC) and provides reasonable assurance and advice to the board and management as to the adequacy and effectiveness of the bank's risk management, controls and governance processes.

In line with an annual risk based audit plan, IA conducts audits of key risk areas of the bank's operations at branches and head office, and issues recommendations to improve risk management, controls and governance processes. All audit action items are tracked through the IA function with a view to ensure that they are closed in a timely fashion.

IA function went through an external quality assessment by an independent and qualified assessor who suggested that AI function performs audits in line with Institute of Internal Auditors (IIA) standards.

Outlook

The economy is expected to remain buoyant in 2014, with growth remaining in the 7% p.a. bracket. Strong private consumption is a key driver to the economy, but remains dependent on possible adverse developments in agriculture and food prices.

In line with reducing inflation, there is a growing possibility of somewhat looser monetary policy in 2014, though possible resulting pressure on the TZS exchange rate may temper this. Also, opening of the capital account within the East African Community may start having an impact on interest rates in future.

inayoendelea ya kukarabati majengo ya matawi pia itasaidia kuboresha sehemu ambapo waajiriwa wetu wanafanyia kazi.

- **Kitengo chetu cha Fedha** kimepewa jukumu la kutengeneza taarifa sahihi za kifedha kwa ajili ya kutayarisha hesabu ya kahasibu na kutoa taarifa, pia kwa ajili ya kusaidia idara nyingine kupata taarifa ambazo zitawasaidia kufanya kazi zao.

Mwaka 2013 kitengo cha fedha kilitambuliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kwa kutayarisha Taarifa za Fedha zilizoandikwa vizuri zaidi na taasisi ya kifedha nchini. Kwa mara nyingine tena, NMB ilitambuliwa na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) kama mmoja wa walipakodi wakubwa na bora. Jitihada zinafanywa kuendelea kuboresha mfumo wa kusimamia taarifa (MIS) ambayo inasaidia mikakati ya kibiashara ya vitengo mbalimbali.

- Kitengo cha **Udhibiti wa Athari** (Risk) kinafanya usimamizi na udhibiti wa kujitegemea kuzuia mazingira yanayoweza kusababisha hasara kwa shughuli za utendaji kibenki kwenye mikopo, masoko, uzingatiaji wa sheria na hatari nyingine. Sera zetu thabiti za kukabili athari zimepelekea kuwepo kwa kiwango kidogo cha mikopo chechefu na uwiano mkubwa zaidi kwa uwezo wa benki kukabiliana na mikopo isiyolipika. Lakini nyuma ya namba hizi kumekuwa na mikakati kabambe ya kuendelea kuboresha mazingira ya kudhibiti athari.

Pia tumeimarisha timu yetu ya kudhibiti athari katika soko, na kuunda timu maalumu ya kusimamia mikopo inayohitaji usimamizi maalumu (SAM). Katika kusimamia mikopo, tunategeneza vigezo vipya, na kuboresha ufanisi wetu kwa kuwa na kitengo kikuu cha kushughulikia mikopo (central loan processing unit). Udhibiti wa Fedha Haramu (AML) na Mjue Mteja Wako (KYC) yamebakia kuwa maeneo yanayotazamwa sana na tunaelekea kuvifikia viwango vipya vya KYC vilivyoweka na Serikali. Hii inasaidiwa pia na mifumo yetu mipya ya AML iliyobuniwa kuboresha jinsi ya kutambua miamala inayotia shaka. Benki imeingia kwenye mradi wa miaka mingi unaojulikana kama Enterprise Risk Management (ERM) ili kulifanya suala la udhibiti wa hasara kama suala la lazima kiutendaji kwenye maeneo yote ya benki.

- Kitengo cha **Ukaguzi wa Ndani** (IA) kinaripoti kwa Bodi ya Wakurugenzi kupitia Kamati ya Bodi ya Ukaguzi na Usimamizi (BARCC) na kinatoa uhakika na ushauri kwa wakurugenzi na menejimenti kuhusiana na uwezo wa benki kudhibiti michakato inayoweza kuleta hatari, michakato ya udhibiti na utawala.

- Kufuatana na mpango wa mwaka wa ukaguzi, IA inafanya ukaguzi wa maeneo muhimu katika operesheni za benki kwenye matawi na makao makuu, na inatoa mapendekezo kuboresha michakato ya udhibiti wa athari, udhibiti na tawala. Maeneo yote ambayo kaguzi mbalimbali zimeonyesha yanahitaji maboresho yanafuatiliwa na IA ili kuhakikisha yanaboreshwa katika muda unaotakiwa.

Strong economic growth rates usually translate in attractive growth rates for the country's leading banks, including NMB. Key dependencies that may have an impact on NMB in the course of 2014 may include:

- The endowment effect of possible downward adjustment in interest rates, which could have an adverse impact on the bank's interest income
- Price volatility on some key commodities including gold and crude oil, and key agricultural commodities such as tobacco, cashew that have a direct impact on the Tanzanian external position, and on NMB's key customer segments.
- The possible consequences of the United States Federal Reserve's "tapering" initiative, which already has had an impact on other countries with high dual current account and fiscal deficits.
- Increased competition from new banking entrants and Mobile Network Operators, both at the top and at the bottom of the banking markets.
- The risks associated with customer segments or products that are an inherent part of our business, including from loan portfolio deterioration, operational and fraud risks or otherwise.

Based on NMB's strong financial position and results, and based on its broad mix of wholesale, SME, agriculture and personal banking customers, supported by appropriate "bricks and mortar" and alternative distribution channels, powered by a strong technology platform, the bank is well positioned to take advantage of the opportunities in the growing Tanzanian market and should be able to withstand possible adverse developments.

Barring unforeseen circumstances, we are therefore looking forward to the future with confidence.



Mark Wiessing
CEO

Matarajio

Uchumi unategemewa kuendelea kukua vizuri mwaka 2014, ukuaji ukibakia ndani ya asilimia 7 kwa mwaka. Matumizi makubwa binafsi ndiyo yatakayoendesha uchumi, iwapo hakutakuwa na maendeleo hasi kwenye kilimo na bei za chakula.

Sambamba na kupungua kwa mfumuko wa bei, kuna uwezekano mkubwa wa kulegezwa kwa sera ya fedha mwaka 2014, ingawa shinikizo linaloweza kutokea kwenye kiwango cha kubadilisha TZS kunaweza kuathiri hili. Pia, ufunguzi wa akaunti za Mitaji (capital account) ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki unaweza kuanza kuwa na athari kwa viwango vya riba katika siku zijazo.

Viwango vya juu vya ukuaji wa uchumi pia hupelekea viwango vizuri vya ukuaji kwa mabanki makubwa nchini, ikiwemo NMB.

Vitegemezi muhimu ambavyo vitakuwa na athari kwa NMB katika mwaka 2014 vinajumuisha:

- Utamaduni tarajiwa wa kuendelea kupunguza viwango vya riba, ambayo ina madhara hasi kwenye mapato ya benki yanayotokana na riba.
- Kuyumba kwa bei za bidhaa muhimu kama dhahabu na mafuta ghafi na mazao muhimu ya kilimo kama tumbaku, korosho ambayo itaathiri moja kwa moja nafasi ya Tanzania katika biashara ya nje na kwa makundi muhimu ya wateja wa NMB
- Athari zinazotarajiwa kutokana na mpango wa Benki Kuu ya Marekani (Federal Reserve) unaojulikana kama "tapering" ambao tayari umeshakuwa na athari kwa nchi nyingine ukisababisha nakisi kubwa ya bajeti na pengo kubwa katika pato la nchi.
- Kuongezeka kwa ushindani kutoka kwa benki mpya zinazoanzishwa na makampuni yanayofanya kazi za fedha kama vile usafirishaji wa fedha kwa njia ya mtandao unofanywa na makampuni ya simu.
- Athari zinazohusiana na makundi ya wateja au bidhaa ambazo ni sehemu ya asili ya biashara yetu, ikiwemo kudorora kwa vitabu vya mikopo, hatari kwenye operesheni za benki na udanganyifu

Kufuatia hali imara ya kifedha ya NMB na kutokana na mchanganyiko wake mpana wa biashara ya jumla, SME, kilimo na wateja binafsi, ikisaidiwa na matawi na njia mbadala za kutolea huduma, zikiendeshwa na mfumo imara wa teknolojia, benki iko kaika nafasi nzuri kunufaika na fursa kwenye soko linalokua la Tanzania na itaweza kustahimili matukio hasi yasiyotarajiwa.

Pamoja na mazingira yasiyotarajiwa, tunautazama mustakabali wetu kwa kujiamini.



Mark Wiessing
Mtendaji Mkuu



We believe in adopting the best practices in Corporate Governance. The Board, Management and NMB employees are committed to upholding the core values of transparency, integrity, honesty and accountability, which are fundamental to the attainment of good governance and excellent performance in any organisation.

Good corporate governance principles are accepted as the drivers of improved corporate performance throughout the world. Responsibility for overseeing the proper implementation of good corporate governance rests with the directors.

NMB tunaamini katika kufuata kanuni za Utawala Bora. Bodi, Uongozi na wafanyakazi wa NMB wamejipanga kusimamia maadili ya msingi ya ukweli na uwazi, uadilifu, uaminifu na uwajibikaji ambayo ni ya msingi ili kuwa na utawala bora na utendaji mzuri katika taasisi yoyote.

Misingi ya utawala bora inakubalika kuwa kichocheo cha utendaji mzuri wa makampuni duniani kote. Jukumu la kusimamia utekelezaji mzuri wa utawala bora liko chini ya Wakurugenzi.



The Board of Directors

■ Functions

The Board is responsible and accountable for providing effective corporate governance, direction and control of the company. The directors have a duty to exercise leadership, enterprise, integrity and judgment based on transparency, fairness, accountability and responsibility.

The Board is responsible for appointing Management, adopting a corporate strategy, policies, procedures and monitoring operational performance including identifying risks impacting the company. It is also responsible for managing good relationships with all stakeholders.

■ Composition

In 2013 the Board of Directors was made up of eight non-executive directors with a mix of skills, experience and diversity. Currently, there is one vacancy on the Board of Directors.

■ Appointment

The appointment of directors is regulated by the Memorandum and Articles of Association of the Company, as well as the guidelines issued by the Bank of Tanzania (BOT) and the Capital Markets and Securities Authority, pursuant to the Banking and Financial Institutions Act 2006 and the Capital Markets and Securities Act 1994, respectively. Shareholders with more than a 10% stake in the share capital of NMB are entitled to nominate one director for every 10% of the shares held by them. The names are presented to the AGM for ratification and appointments are submitted to BOT for approval.

All non-executive directors are subject to retirement by rotation and re-election by shareholders periodically in accordance with the articles of association. Rotation is staggered to ensure continuity of experience and knowledge. The number of terms an individual may serve is not limited. The Companies Act 2002 requires that directors retire at the age of 70 years, however there is a provision in the law for re-election.

■ Resignations

At the AGM held in June 2013, Directors William Mlaki and Margaret Ikongo tendered their resignations to the Board after completing their terms. They were both re-appointed as directors for a further three year term.

■ Board meetings

The Board meets quarterly, with additional meetings convened as and when necessary.

During 2013, the Board and its committees met to discuss and decide on the business activities. The Board Committees act on behalf of the Board to direct the bank effectively and accelerate the decision-making process. The four Board

Bodi ya Wakurugenzi

■ Majukumu

Bodi ina jukumu la kusimamia na inawajibika kuwa na utawala bora wenye ufanisi kwa kutoa uongozo na uthibiti wa kampuni. Wakurugenzi wa Bodi wana jukumu la kuonyesha uongozi mahiri, uelewa wa kibiashara ya benki, uadilifu na kutoa maamuzi kwa msingi wa uwazi, haki na uwajibikaji. Bodi ina majukumu ya kuchagua uongozi, kuweka mkakati wa kiuongozi wa biashara, sera, taratibu na mipango ya ufuatiliaji wa utendaji, ikiwa ni pamoja na kutambua athari zinazoikabili benki. Bodi pia ina jukumu la kusimamia mahusiano mazuri na Wadau wote wa benki.

■ Wajumbe

Mwaka 2013 Bodi ya Wakurugenzi ilikuwa na Wakurugenzi nane wasio watendaji wote wakiwa na ujuzi na uelewa wa mambo mbalimbali. Kwa sasa kuna nafasi moja kwenye Bodi ya Wakurugenzi.

■ Uteuzi

Uteuzi wa Wakurugenzi wa Bodi ya NMB unaongozwa na sheria ya benki (Memorandum and Articles of Association) na miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Tanzania kulingana na sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994. Wanahisa walio na hisa zaidi ya asilimia 10 wanaruhusiwa kuchagua mkurugenzi mmoja kwa kila asilimia 10 ya hisa wanazozimiliki. Majina yanawakilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa kwa kupitishwa. Uteuzi wao huwasilishwa Benki Kuu ya Tanzania ili kupata kibali.

Wakurugenzi wote wasio watendaji wanatakiwa kustaafu kwa mzunguko na kuchaguliwa tena na wanahisa kwa vipindi kulingana na muongozo na sheria za Benki. Mzunguko huu ni muhimu ili kuhakikisha muendelezo wa kumbukumbu ya kitaasisi na kuleta ujuzi na uzoefu mpya. Miaka ya kuwa Mkurugenzi haina kikomo. Sheria za Makampuni ya mwaka 2002 inahitaji mkurugenzi astaafu akiwa na miaka 70 ila sheria inaruhusu pia mkurugenzi huyo kuchaguliwa tena.

■ Kujiuzulu

Kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka ulofanyika Juni 2013, Wakurugenzi William Mlaki na Margaret Ikongo waliwasilisha hoja ya kujiuzulu kwenye Bodi baada ya kumaliza muda wao. Wote wawili waliteuliwa tena kuwa Wakurugenzi kwa kipindi cha miaka mitatu mingine.

■ Vikao vya Bodi

Bodi inakutana kila baada ya miezi mitatu na vikao vingine vinaitishwa ikilazimu. Mwaka 2013 Bodi na kamati zake zilikutana kujadili na kuamua maswala na shughuli za kibiashara. Kamati za Bodi zinatenda kwa niaba ya Bodi

committees are: the Board Executive Committee (BEC), the Board Audit, Risk and Compliance Committee (BARCC), the Board Human Resources and Remuneration Committee (BHRC) and the Board Credit Committee (BCC).

The number of meetings held over the course of the year is given in brackets:

- Board of Directors (6)
- Board Executive Committee (6)
- Board Audit Risk and Compliance Committee (4)
- Board Human Resources and Remuneration Committee(5)
- Board Credit Committee (14)

Members of the Board and respective committees as at 31st December 2013 are shown in the table below:

S/No.	Name Jina	Main Board Bodi Kuu	BEC ¹ Kamati ya Utendaji	BARCC ² Kamati ya Ukaguzi, Athari na Utilifu	BCC ³ Kamati ya Mikopo	BHRC ⁴ Kamati ya Rasilimali Watu na Maslahi
1.	Joseph Semboja	Chairman Mwenyekiti	Chairman Mwenyekiti			
2.	Anne Mbughuni	Member Mjumbe		Member Mjumbe	Member Mjumbe	
3.	Albert Jonkergouw	Member Mjumbe	Member Mjumbe		Member Mjumbe	Member Mjumbe
4.	Jos van Lange	Member Mjumbe		Chairman Mwenyekiti		
5.	Mike Laiser	Member Mjumbe	Member Mjumbe	Member Mjumbe		Chairman Mwenyekiti
6.	Protase Tehingisa	Member Mjumbe			Member Mjumbe	Member Mjumbe
7.	Margaret Ikongo	Member Mjumbe				Member Mjumbe
8.	William Mlaki	Member Mjumbe		Member Mjumbe	Chairman Mwenyekiti	

¹ BEC (Board Executive Committee)

² BARCC (Board Audit, Risk and Compliance Committee)

³ BCC (Board Credit Committee)

⁴ BHR&RC (Board Human Resources and Remuneration Committee)

kuelekeza benki kwa usahihi na kuchochea mchakato wa kufanya maamuzi. Kamati nne za Bodi ni: Kamati ya Wakurugenzi, Kamati ya Ukaguzi, Athari na Utilifu, Kamati ya Rasilimali Watu na Maslahi na Kamati ya Mikopo.

Namba ya vikao vilivyofanyika mwaka uliopita vinaonekana kwenye mabano:

- Bodi ya Wakurugenzi (6)
- Kamati ya Utendaji (6)
- Kamati ya Ukaguzi, Athari na Utilifu (4)
- Kamati ya Rasilimali Watu na Maslahi (5)
- Kamati ya Mikopo (14)

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na kamati husika kufikia tarehe 31 Disemba 2013 ilikuwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

■ Directors Evaluation

The Board itself regularly undergoes self-assessment and evaluation under the guidance of an independent party in order to improve the internal Governance of the Board and its Committees.

■ Relationship with Auditors

The Board Audit, Risk and Compliance Committee and the full Board held meetings with the external auditors to discuss these auditors' terms of engagement, duties and various other issues during the year under review.

Board Committees

■ Board Executive Committee

The Committee assists the Board in fulfilling its oversight responsibilities in accordance with the Articles of Association of the Company. The Committee exercises the powers of the Board in managing the business and affairs of the Company during the intervals between Board meetings, when action by the Board is necessary or desirable but convening a special Board meeting is not warranted or practical.

■ Board Audit, Risk and Compliance Committee

The Committee assists the Board in fulfilling its oversight responsibility relating to the integrity of the bank's financial statements and financial reporting process, systems of accounting and financial controls; the annual external audit of financial statements, reporting and internal controls; performance of the Internal Audit, Risk and Compliance Functions; compliance with legal and regulatory requirements; adequacy of the risk management function; the oversight responsibility on planning and conduct of audits to determine that the bank's financial statements and disclosures are complete and accurate and are in accordance with International Financial Reporting Standards and applicable laws, rules and regulations.

■ Board Human Resources & Remuneration Committee

